

**MAZOEZI****JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA BURETI****KISWAHILI****INSHA****102/1****KARATASI LA KWANZA****1. LAZIMA**

Wewe ni mkenya. Umefuzu shahada ya ukapera na uzamili, na kuajiriwa kazi katika idara ya forodha. Andika TAWASIFU yako.

2. Eleza juhudi ambazo serikali imefanya kushirikisha vijana katika ujenzi wa taifa.

3. Andika insha kuthibitisha methali. Mtaka cha mvunguni sharti ainame.

4. tunga kisa kinachomalizikia kwa maneno yafuatayo:

.... Mhadhiri mkuu wa kitivo alipoita jina langu, nilishusha pumzi, kweli safari imekuwa ndefu.

**JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA BURETI****KISWAHILI****102/2****LUGHA****KARATASI LA PILI****1. UFAHAMU****Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Tokea muundo mpya wa serikali ya ugatuzi uanze kutekelezwa miaka miwili iliyopita, kumeendelea kushuhudiwa matatizo mengi hali iliyopelekea kushuhudiwa kwa msururu wa migomo na maandamano ya raia. Fujo za karibuni kabisa mizile zinazoshuhudiwa katika miji mikubwa za wachuuzi na wafanyibiashara wakipiga hatua za serikali za kaunti kuwatoza ushuru takribani kwa kila huduma na bidhaa ikiwemo wanyama, kuku na ndege. La kuhuzunisha zaidi katika baadhi ya majimbo imeripotiwa kuwa raia wamelazimishwa kulipwa ushuru kwa kutaka tu kuona maiti za jamaa zao kwenye vyumba vya kuhifadhia maiti!

Wanasiasa wameonekana kuwa na wakati mgumu kutetea mfumo huu mpya wa ugatuzi huku baadhi wakisema kwamba matatizo yanayoshuhudiwa kwa sasa yametokana na ugeni wa mfumo huo. Wengine wameinyoshea kidole serikali ya kitaifa kwamba ndiyo inayosambaratisha muundo huu. Wengine wanahoji kuwa bado ni mapema na kwamba kunahitajika muda mrefu ili kufaulu.

Ni wazi kwamba kumekosekana nidhamu bora ya kusimamia maisha ya raia nchini Kenya. Matatizo yanakumba raia kwa sasa ni dalili kuwa mfumo wa serikali ya ugatuzi umeongezea chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu. Swali ni je, hadi lini nidhamu ya kusimamia raia itakuwa ni Suala la majaribio na makosa?

Hatua ya kuwarundikizia raia ushuru mkubwa ni kitendo cha unyonyaji na cha dhuluma kinachofaa kupingwa. La kufahamishwa hapa ni kwamba ushuru ndio njia kubwa ya kuzalisha mapato ya serikali zinazojifunga na mfumo wa kimagaribi wa kiuchumi wa kibepari ikiwemo Kenya. Asilimia 90 ya mapato ya serikali za kibepari huegemea ushuru. Kwa hivyo hatua ya serikali za kaunti katika kuwanyonya raia kwa kuwalipisha ushuru si ajabu bali ni thibitisho kuwa jamii ya Kenya inaongozwa na nidhamu ya kiuchumi ya ubepari mfumo wa unyonyaji na Ukandamizaji. Ukweli unabakia kuwa ndani ya serikali za kibepari raia ndio hubebeshwa mzigo wa ushuru unaoishia matumboni mwa viongozi!

Miito ya mabadiliko ya katiba na ya miundo mipya ya kiutawala si yoyote ila ni moja tu ya hatua za mfumo wa kibepari kujipa muda wa kuishi na kuziba aibu zake za kushindwa kusimamia maisha ya watu. Kufeli huku kwa mfumo huu kunashuhudiwa hadi kwenye nchi kubwa za kibepari kama Marekani na Uingereza hivyo nazo zimekumbwa tele na maandamano na fujo za raia wakilalamikia hali ngumu ya maisha.

**Maswali**

- |  |           |
|--|-----------|
| a) Yape makala haya anwani mwafaka.  | (alama 1) |
| b) Eleza mtazamo wa Wanasiasa kuhusu utepetevu wa mfumo huu.                                 | (alama 3) |
| c) "Ugatuzi nchini Kenya ni mfumo wa kibepari" thibitisha kauli hili kwa kurejelea makala.   | (alama 4) |
| d) Kulingana na taarifa uliyosoma, nini chanzo cha misururu ya migomo na maandamano ya raia? | (alama 3) |
| e) Thibitisha jinsi mfumo wa ugatuzi umeongeza chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu.       | (alama 2) |
| f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa hii.                    | (alama 2) |
| i) Ugatuzi   |           |
| ii) Kibepari   |           |

## 2. UFUPISHO

Tunapinga na kulaani vikali visa vya ugaidi vinavyoendelea kutetemesha usalama wa wananchi. Hivi ni vitendo vya kinyama vinavyotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu na utu kabisa. Inakera mno kwa vitendo vya kigaidi. Inagadhambisha kuona wakenya wasio na makosa wakiteswa na kuuwawa kinyama bila huruma na watu wasio na utu. Hatuogopi wala hatuna fedheha kuamba magaidi hawa wamelaaniwa na siku zao zimehesabiwa hapa duniani, damu yam wananchi asiye na makosa katu watailipia. Napinga vikali pale magaidi hawa wanapohusisha vitendo hivi kuwa vita vya kidini, vita hivi si vya kidini kwani hakuna dini yoyote iliyo na Imani ya kumwua kinyama binadamu asiye na makosa.

Kando na tishio la ugaidi, wakenya pia wanakabiliwa na hatari za ujambazi, mauaji, unajisi, ubakaji na maovu mengine. Katika juhudi za kudumisha usalama, polisi wana jukumu la kutumia kila Mbinu kuhakikisha kuwa haki ya kikatiba ya wakenya kuhusu kulindwa kwa maisha na mali yao. Lakini cha kusikitisha ni kuwa, Mbinu ambazo polisi wamekuwa wakitumia hasa ile ya kufanya misako inayoishia kuwanasa mamia ya raia wasio na habari kinachoendelea, inawaongezea wakenya mateso. hali hii inawaacha kwenye hatari ya kunaswa na majambazi ama polisi.

Matumizi ya Mbinu hii ya misako imeishia kunasa raia wengi wasio na makosa. Wanapaswa, hurundikwa kwenye seli usiku mzima ama siku kadha na hata kama wanaachiliwa huwa tayari wameteseka. Huu ni ukiukaji wa haki za raia. Kadhalika, Mbinu hii yaonekana kama hila ya polisi kutaka kuonyesha wanafanya kazi lakini sio mwafaka kwani wanapokuwa wakiwanasa raia mijini na mitaani, magaidi na majambazi wanaendelea na shughuli zao.

Badala ya kusaka wakora kwa kubahatisha kwenye umati, polisi wanapaswa kubuni njia ambazo zitawapa mwelekeo mwafaka zaidi kuhusu wahalifu ili waweze kuwafuatilia. Ushirikiano baina yao na majasusi uwepo. Hii itawezesha polisi kupata habari muhimu kuhusu vitisho vya uhalifu. Maafisa wa usalama pia wanaweza kupata habari muhimu kutoka kwa raia.

i) Ni nini maoni ya mwandishi kuhusu Suala la ugaidi. (maneno 60-70) (alama 7, 1 utiririko)

ii) Kwa kutumika maneno yasiyozidi 50 fupisha aya mbili za mwisho. (alama 6, 1 utiririko)

## 3. MATUMIZI YA LUGHA

a) Onyesha tofauti zilizopo kati ya

i) /e/

ii) /u/

(alama 2)

b) Ainisha viambishi katika neno waliibiana

(alama 2)

c) Tambua matumizi ya kiambishi ji katika sentensi ifuatayo.

(alama 2)

Jino la jitu lililiwezesha kujilia chakula kingi kuliko mkimbiaji yule

d) Taja vigezo vitatu vya kuainisha sauti za irabu.

(alama 3)

e) Andika kinyume cha sentensi hii

Baba amejenga nyumba nzuri iliyosifiwa na mgeni

f) Eleza tofauti ya kisarufi ya maneno yaliyopigiwa mstari

(alama 2)

i) Hiki ni kitabu cha mwalimu

ii) Hikini cha mwalimu

g) Tunga sentensi kuonyesha matumizi mawili ya kistari kifupi (-)

(alama 4)

h) Andika katika usemi wa taarifa

'Mbona unamfanyia karaha mwenzako? Je, utaenda kumwomba radhi? Phanice aliuliza.

i) Tumia maneno yafuatayo katika sentensi moja ili kubainisha tofauti zao kimaana:

(alama 2)

i) Chuuza

ii) Chuza

j) Eleza maana mbili katika sentensi hii.

(alama 2)

Majambazi walimwibia Letangule gari jipya

k) Andika kwa ukubwa

Kiti kilichokuwa kimekaliwa na mwanamke yule kilivunjika.

(alama 2)

l) Bainisha vielezi na ueleze ni vya aina gani katika sentensi hii.

(alama 2)

Sipendi wanaohama kwao ili kuenda kuishi kizungu.

m) Akifisha:

rais alimwamuru usiwashughulikia mabalozi wajeuri

(alama 3)

n) Tambua shamirisho katika sentensi ifuatayo:

(alama 2)

Mwalimu mkuu alituanalia karamu ya kufana

o) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi mawili ya kiambishi ndi-

(alama 2)

p) i) Ainisha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia jukumu lake

(alama 1)

ii) Tunga sentensi moja ya kuonyesha rai

(alama 1)

q) Weka kirejeshi 'O' tamati kwenye kitenzi **chungu** kisha ukitungie sentensi.

(alama 1)

r) Nomino hizi ziko katika ngeli gani?

(alama 2)

## 4. ISIMU JAMII

Maenezi ya Kiswahili Afrika Mashariki punde baada ya uhuru yalikuwa na mchango tele.

Fafanua zozote tano.

(alama 10)

**JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA BURETI****KISWAHILI****102/3****KARATASI YA TATU****FASII****SEHEMU YA A****1. Lazima**

Onyesha namna mwandishi wa Kidagaa Kimemwozea amefaulu kutumika Mbinu zifuatazo.

a) Kiangaza mbele (alama 10)

b) Stihizai (alama 10)

**SEHEMU YA B****Tamthlia ya Mstahiki Meya: Timothy Arege****Jibu swali la 2 au 3****2. "Iwapo umefanya yapo mengi ambayo hayakunyooka."**

a) Andika muktadha wa dondo. (alama 4)

b) Eleza jinsi baadhi ya wahusika walivyojaribu kuyanyoosha mambo. (alama 6)

c) Dhihirisha unadhirifu katika tamthlia ya Mstahiki Meya. (alama 10)

**AU****3. Hatua tuchukuazo maishani mwetu zaweza kutuathiri na kuathiri nchi pakubwa. Fafanua kauli hii ukimrejelea Meya Sosi. (Hoja kumi)****SEHEMU C: USHAIRI****Jibu swali la 4 au la 5****4. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.****Amiri A.S Andanenga: Sauti ya Kiza**

1. Ngakua na mato, ya kuonea  
Ngalisana kito, cha kuchezea  
Kilicho kizito, cha kuelea  
Kikamuenea, akivae

2. makusudi yangu, ngaliandaa  
Ngafinyanga chungu, cha mduwaa  
Ngatia vitangu, vinavong'aa  
Ili ziwe taa, kwa apikae

3. Mkungu wa tano, wa mduwara  
Ulo bora mno, kisha imara  
Ulo na maono, kuwa ni dira  
Kwenye barabra, itindiae

4. Ngaomba baraka, kwake Rabana  
Punje za nafaka, kila aina  
Chunguni kuweka, kwa kulingana  
Hajaangu suma, yule alae

5. Ngafanya bidii, kwenda mwituni  
Sio kutalii kukata kuni  
Ya miti mitii, huko jikoni  
Isio na kani, ni iwakae

6. Kwa yangu mabega, nikathubutu  
Ngabeba mafiga, yalo matatu  
Bila hata woga, kwenye misitu  
Samba tembo chatu, sinitishie

7. Miti yenye pindi, na jema umbo  
Ngajenga ulindi, mwemw wimbombo  
Fundi aso fundi, penye kiwambo  
Moyo wake tambo, apekechae

8. Singaajiri, ngachimba mimi  
Kisima kizuri, cha chemchemi  
Maji ya fahari, ya uzizini  
Jua la ukami, siyaishae

9. Tamati nafunga, kwa kuishia  
Mato ndo malenga, kanikimbia  
Nahofu kutungwa, mabeti mia  
Asije chukia, ayasomae

- a) Eleza ujumbe wa shairi hili. (alama 2)
- b) Kwa kurejelea ubeti wa pili, eleza umuhimu wa aina mbili za uhuru wa kishairi aliyotumia mshairi. (alama 4)
- c) Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- d) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)
- e) Fafanua aina tatu za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 6)
- f) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 2)

5. **Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.**

1. Sema simea wajibu, mwenye kutetema,  
Sema na walo karibu, mbali ukisema,  
Sema kufunza wajibu, noleji, hekima,  
Sema ajue Fulani, usihulu sema
2. Sema yanayokukaa, yanakusakama,  
Sema yaliyozagaa, kwa mwako mtima,  
Sema unajihadaa, kwani tawafuma?  
Sema wajue ni nani, usiache sema
3. Sema yote si uasi, si tenge si noma,  
Sema toa wasiwasi, upate salama,  
Sema japo ni risasi, longi litauma,  
Sema yote hadharani, radidia sema
4. Sema pasi na ukali, mwiza taloloma,  
Sema neno la asali 'taramba' kitema,  
Sema kwa mzo akili, watakushituma,  
Sema kwa yako maghani, usikome sema
5. Sema zitaje ghururi, duniya ni dema,  
Sema ana maghubari, duniya ni rima,  
Sema duniya hatari, mwina wa nakama,  
Sema sema kwa yakini, masa ghaya sema
6. Sema 'kwani hamuoni, waloachwa nyuma?'  
Sema pasi taraghani, uliyoyasema,  
Sema wachuma tumboni, ja minyoo sema,  
Sema sema mwafulani, u salama sem

**Maswali**

- a) Toa mifano miwili ya idhini ya kishairi katika shairi hili. (alama 2)
- b) Tambua bahari zozote nne zinazopatikana katika shairi hili na utoe sababu. (alama 4)
- c) Onyesha vile shaha alivyofua dafu katika kutumia Mbinu zifuatazo: (alama 2)
- i) Anafora
  - ii) Usambamba wa kiusawe
- d) Eleza toni ya shairi hili. (alama 2)
- e) Ujumbe wa nafsineni unamlenga nani? (alama 2)
- f) Eleza sifa za kiarudhi katika ubeti wa pili. (alama 4)
- g) Andika ubeti wa tano katika lugha tutumbi/nathari. (alama 4)

**SEHEMU YA D**

**Hadithi fupi: Damu nyeusi na hadithi nyingine**

6. Huku ukirejelea hadithi zifuatazo, jadili maudhui ya ukengeushi
- i) Mke wangu
  - ii) Samaki wa nchi za joto
  - iii) Damu nyeusi
  - iv) Tazamana na mauti

**SEHEMU YA E**

**Fasihi simulizi**

7. a) Taja tanzu zozote tano za Fasihi simulizi kisha utoe mifano miwili ya vipera vyake. (alama 10)
- b) Eleza sifa zozote tano ambazo hupote Fasihi simulizi inapoandikwa. (alama 5)
- c) Miviga ni nini? (alama 1)
- d) Fafanua sifa nne za miviga. (alama 4)